**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

**SALAMU ZA HALMASHAURI YA WALEI PAROKIA - HERI YA MWAKA MPYA 2026**

Mheshimiwa Baba Paroko,

Waheshimiwa Mapadre,

Makatekista,

Wana Halmashauri ya Walei Parokia,

Waamini wote wana Kung'ara kwa Yesu Kristo, Mbezi Mshikamano,

Tumsifuni Yesu Kristo.

## SHUKRANI KWA 2025

Tumemaliza mwaka 2025 na tunaingia mwaka mpya 2026, kwa kuangalia ni mwendelezo wa saa zilezile, saa 24 kwa siku, na siku zilezile 7 za wiki, lakini zikiwa na mabadiliko na maana kubwa katika mipango na maisha ya mwanadamu, hasa anayemwamini Mungu.

Tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa yote aliyotujalia, kubwa ikiwepo pumzi ya uhai katika mwaka 2025. Hii ni kuanzia mtu mmoja mmoja, familia, Jumuiya na Parokia kwa ujumla. Ulikuwa mwaka wenye changamoto kadhaa kwa mtu binafsi, mpaka taifa na ulimwengu mzima. Tunamshukuru sana Mungu kuzivuka changamoto zote salama.

## MAFANIKO YA 2025

Mwaka 2025 Mungu alitukirimia makubwa kama Parokia kuanzia utoaji wa sakramenti mbalimbali, ushiriki na uandaaji wa mafungo, semina na Hija, ukamilishaji nyumba ya mapadre na kuizindua (vimebaki vitu vichache), kuzindua Tovuti ya Parokia na Jubilei ya miaka 10 ya Parokia (itakayohitimishwa mwaka huu mpya 2026).

Pia uboreshaji wa mafundisho ya watoto kwa kuanzisha darasa la Jumapili (Sunday school) na utoaji chai na mafundisho ya Komunio na Kipaimara yaliyofanya ongezeko la watoto katika Misa za watoto kutoka wastani wa 250 mpaka 470 hivi.

Kadhalika tumekuwa katika mwaka wa uchaguzi wa viongozi wa Halmashauri ya Walei Parokia kuanzia ngazi ya Jumuiya ambapo sasa tumekamilisha ngazi ya Parokia kwa Vyama vya Kitume na kuelekea kukamilishwa na uchaguzi wa Kamati Tendaji Parokia 01.03.2026 kwa kadiri ya ratiba ya uchaguzi ya Jimbo. Viongozi wote sasa tuna wajibu wa kutambua na kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi kwa maendeleo ya Kanisa la Kristo.

Kwa haya machance yaliyotajwa tuna kila sababu ya kumuambia Mungu aksante. Tunawashukuru sana Baba Paroko na mapadre wetu kwa miongozo na Baraka zao katika kuyafanikisha. Tunawashukuru viongozi na waamini wote waliochangia kufanikisha. Tunaendelea kuomba tena ushirikiano wenu kwa mwaka huu mpya 2026.

**VIPAUMBELE VYA 2026**

Vipaumbele vya Parokia 2026 vipo vingi lakini tutataja kwa uchache.

Tunataraji kuboresha Liturujia na maadhimisho mbalimbali, kukamilisha taratibu za ujio wa Masista ili kuimarisha huduma na mafundisho hasa kwa watoto na vijana.

Uimarishaji wa familia, Jumuiya na Vyama na Mashirika ya Kitume pamoja na kutembelea Jumuiya zote za Parokia. Uboreshaji Kamati mbalimbali na. Kuhimiza ndoa kwa wanaoishi bila ndoa pamoja na uboreshaji wa mafundisho endelevu.

Kumalizia Kanisa (feni, rangi, kinanda), kamilisha ukumbi wa Parokia, madarasa ya watoto, ujenzi wa uzio wa eneo la Parokia na mageti, na kumalizia sehemu zilizobaki nyumba ya mapadre. Pia uhamishaji na uboreshaji wa vyoo kutoka vilipo, na kufanya sehemu hiyo kuwa ofisi za Halmashauri na Vyama vya Kitume. Orodha kamili na ratiba ya utekelezaji itatolewa kupitia Halmashauri ya Walei Parokia.

**UJUMBE WA PAPA KWA SIKU YA AMANI**

*Katika Ujumbe wa Papa Leo XIV kwa Siku ya 59 ya Amani Duniani 01.01.2026 unaoongozwa na kauli mbiu: "Amani iwe nanyi nyote, kuelekea amani isiyo na silaha inayoondoa Silaha,"*

*Hii ndiyo amani ya Kristo Mfufuka, amani isiyo na silaha na amani inayoondoa silaha, nyenyekevu na vumilivu. Inakuja kutoka kwa Mungu. Mungu ambaye anapenda bila kulazimisha.*

*Kristo, amani yetu, ambaye ameshinda kifo na kubomoa kuta za mgawanyiko zinazotenganisha ubinadamu (Efe 2:14). Ili kushinda giza, ni muhimu kuona Nuru na kuiamini. Nuru hiyo ndiyo Kristo Mwenyewe.*

*Papa anasema ulimwenguni kote, inatarajiwa kwamba "kila jamii iwe 'nyumba ya amani,' ambapo mtu hujifunza jinsi ya kupunguza uadui kupitia mazungumzo, ambapo haki inatekelezwa na msamaha unathaminiwa."*

**HITIMISHO**

Kwa kuzingatia mwaliko wa siku ya Amani, tunaalikwa tuungane katika Neno la Mungu (Flp 4:7-9) *Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo. Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.*

Kama wana Parokia, tunaalikwa sote kuwa wajumbe na vyombo vya Amani ya Kristo ili naye akae ndani yetu kwa mwaka 2026.

Tumsifuni Yesu Kristo na Heri ya mwaka mpya 2026.

*Imetolewa na Kamati Tendaji Parokia.*